


JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA



**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**



15/10/2021

T A N G A Z O

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anatangaza Zabuni ya kukodi magari kwa ajili ya Shughuli za Mitihani. Tarehe 28 na 29 Mwezi Oktoba ,2021. Maombi ya zabuni kutoka kwa Watu binafsi,Taasisi mbalimbali na wenye magari yenye sifa zifuatazo yanakaribishwa;-
 - a. Gari liwe ni aina ya "station wagon au hard top"
 - b. Gari liwe na nafasi ya kubeba watu 8 – 12.
 - c. Gari liwe na dereva mwenye leseni iliyo hai na halali.
 - d. Gari liwe na Bima.
 - e. Gari liwe katika hali nzuri ya kukabiliana na milima na mabonde.
2. Maombi kwa waliokidhi sifa zilizotajwa wafike kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)-Nyasa (Kata ya Kilosa) kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri tarehe **15/10/2021 (Ijumaa)** hadi **21/10/2021 (Alhamisi)** kwa ajili ya kuchukua **fomu za maombi**. Fomu za maombi zinapatikana **bila malipo** kutoka ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.

Maombi yaandikwe na kutumwa kwa ;-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa

S.L.P 90. MBAMBA BAY.

4. Kotesheni zote ziwe na nakala mbili (original 1 na copy 1) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Kotesheni Na.

Darasa la nne] Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Kata ya Kilosa (Bomani) S.L.P 90 Mbamba bay.

5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni Alhamisi ya tarehe **21/10/2021** kabla ya Saa tisa na nusu (**9.30**) jioni. Kotesheni zitafunguliwa hadharani kuanzia Saa tisa na nusu (**9.30**) jioni tarehe 21/10/2021 mbele ya waombaji/wawakilishi watakaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa Zabuni katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa [Nyasa bomani] zilizopo Kata ya Kilosa, S.L.P 90, Mbamba bay.
6. **Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa Tathmini(Evaluation).**

➤ **Maelezo zaidi yanapatikana katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi.**


Jimson P. Mhagama

MKURUGENZI MTENDAJI(W)

NYASA

